**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA HANANG.**


SIMU :-
MKUU WA SHULE
**0692507151**
MAKAMU MKUU WA SHULE
**0784954143**
Jorojik@gmail.com

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI JOROJIK,
S.L.P.260,
**KATESH/HANANG,**
**MANYARA.**


TAREHE 15/12/2020

**Kumb. Na. JSS/KDI/20/V.02**

**Jina la mwanafunzi :**________________________________________
**S.L.P:** ____________________________

# YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI JOROJIK WILAYA YA HANANG' MKOA WA MANYARA MWAKA - 2021.

## 1.0 .Utangulizi

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha **KWANZA** katika shule hii ya sekondari Jorojik kwa mwaka wa masomo2021. Shule ya sekondari **JOROJIK** ipo wilaya ya Hanang' Mkoa wa Manyara, upande wa kusini mwa makao makuu ya Mkoa **Manyara (BABATI**). Shule ipo Kata ya **GITTING** kijiji cha **Gitting** kitongoji cha **Malap**u mbali wa **km 28** kaskazini mwa makao makuu ya Halmashauri ya wilaya ya **Hanang'/ KATESH**.

Usafiri wa basi kutoka mjini (makao makuu ya wilaya) **KATESH** unapatikana katika kituo cha mabasi cha **KATESH** Kwa nauli ya **Tsh.2000/=** tu Mpaka stendi ya Gitting. Umbali kutoka stendi ya daladala/ (bodaboda) ya Gitting' mpaka shuleni ni **km 1. Nauli kwa bodaboda ni Tsh 1000/=**

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021**. Unatakiwa kuripoti Shuleni kuanzia tarehe **11/01/2021** na mwisho wa kuripoti ni tarehe **24/01/2021**. Ndani ya siku kumi na nne (**14**) baada ya muhula wa kwanza kuanza.

**HONGERA SANA !!!!!!**

## 2.0 . MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA.

### 2.1 . SARE ZA SHULE.

a) Suruali ya rangi ya **Damu ya mzee** na **Shati jeupe la Mikono mifupi** Kwa Wavulana.

b) Sketi ya rangi ya **Damu ya mzee** na **shati jeupe la mikono mifupi** kwa Wasichana (idadi ni mbili).

c) Sweta la rangi ya **Damu ya mzee** la **(V)** KOLA

d) Soksi za **Kaki** kwa Wavulana na **nyeupe** kwa Wasichana na tai ya rangi ya damu ya mzee

e) Viatu vyeusi vya NGOZI vyenye Kamba na vya kufuta na dawa ya viatu {kiwi} visiwe na kisigino kirefu na visiwe buti.

**AINA YA MSHONO**

- wavulana, Suruali ndefu isio ya kubana yenye serebration na turn up.
- Wasichana sketi ndefu nchi 8 kuanzia kwenye magoti kushuka chini yenye marinda 12 yaani sita mbele na sita nyuma na isiwe ya kubana.
- Rangi ya Hijabu ifanane na Sare za Shule (hijabu iwe njeupe). Isiyo na mapambo yeyote

**NB: ENDAPO MWANAFUNZI ATASHONA TOFAUTI NA MAELEKEZO HAYA MWANAFUNZI HATAPOKELEWA SHULENI**

**SARE ZA MICHEZO KWA SHULE HII NI;**

I. **WAVULANA.**

- Flana (T- shirt 2 za Blue), Bukta 2 za bluena viatu vya michezo pair mbili ni lazima siku ya michezo.
- Track suit rangi duck blue kwaajili ya siku za kazi ya shamba. Pamoja na safari mbalimbali za kimasomo.

II. **WASICHANA.**

- Flana (T-shirt 2 za Blue), Bukta 2 za Blue na viatu vya michezo pair mbili ni lazima siku ya michezo.
- Track suit rang duck blue kwaajili ya siku za kazi ya shamba. Pamoja na safari mbalimbali za kimasomo.

**SIKU YA MICHEZO NILAZIMA WANAFUNZI WOTE WAVAE SARE ZA MICHEZO KAMA MAELEKEZO YALIVYO TOLEWA.**

### 2.2. VIFAA VYA TAALUMA

1. Daftari, kalamu na Mkebe wa hesabu (Daftari counter book two quire- 10) na kijitabu chenye karatasi za vyumba (Graph paper) kwaajili ya mazoezi.
2. Fail la kutunzia kumbukumbu zake mbalimbali awapo hapa shuleni (folder file).
3. Dictionary / kamusi ya kiingereza. (English – English or English – Swahili or Swahili – English)

## 2.3: MICHANGO YA CHAKULA

Chakula cha wanafunzi wa kutwa ni mahindi **debe 4** na maharage **debe 2** na hela kiasi cha Tsh **40,000/=** kwa mwaka. Hii ni sawa na **debe 2** za mahindi na **debe 1** la maharage pamoja na Tsh **20,000/=** kwa muhula. Mahitaji hayo lipia kupitia akaunti ya kamati ya chakula yenye jina la akaunti (**kamati ya chakula Jorojik sekondari** namba **41010006447 (NMB**), kwa mahindi na maharage vitapokelewa shuleni kupitia kamati ya wazazi ya chakula.

## 2.4 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa sheria **Na.25** ya mwaka **1978** na kama ilivyo rekebishwa kwa sheria **Na. 10** ya mwaka **1995**. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu yenye dhamana ya Elimu nchini na Ofisi ya Rais **-TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yata fafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni:

### SHERIA ZA SHULE

a. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.

b. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya Shule ni lazima.

c. Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (Preparation).

d. Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazo pewa.

e. Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika Shule hii.

f. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.

g. Kuvaa sare za Shule wakati wote unapotakiwa Shuleni na nje ya Shule.

h. Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote.

i. Kutunza mali za umma.

### 2.5. Makosa yafuatayo yanaweza kusababisha kufukuzwa au kusimamishwa shule.

a) Wizi.

b) Uasherati na Ushoga.

c) Ubakaji.

d) Ulevi na matumizi ya madawa za kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi **n.k**.

e) Kupigana au kupiga.

f) Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.

g) Kudharau Bendera ya Taifa.

h) Kuwa mjamzito/kupata mimba /Kusababisha mimba.

i) Kuoa au kuolewa.

j) Kutoa mimba.

k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.

l) Kukataa adhabu kwa maksudi.

m) Kuwa na simu ya mkononi.

**3 Mambo Mengine Muhimu yanayo paswa kukamilishwa na kuwasilishwa Shuleni na Mwanafunzi:-**

a) Medica Examination. Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Form hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti Shuleni.

b) Form ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kuto shiriki migomo, fujo na makosa ya jinai.

c) Form ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayo tolewa na Shule.

**3.0 . Tafadhali soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**NB:** Form hii imeambatanishwa na fomu ya vipimo (Medical Examination Form) na Form ya kiapo na makubaliano ya mzazi. Fomu hizo ataziwasilisha zikiwa zimejazwa siku atakapo kuwa anaripoti shuleni. Mawasiliano kwa maelezo zaidi:-

MKUU WA SHULE
**0692507151**
MAKAMU MKUU WA SHULE
**0784 954143**

**KARIBU SANA JOROJIK SEKONDARI.**

THE HEADMISTRESS
JOROJIK SEC-SCHOOL
P.O-BOX 260 KATESH

**SIFA E. MLIGO**

**MKUU WA SHULE.**

PRESDENT'S OFFICE

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNIMENT

HANANG DISTRICT COUNCIL – MANYARA

JOROJIK SECONDARY SCHOOL. *** P.O.BOX. 260 KATESH – HANANG'

**FORM FOR MEDICAL EXAMINATION:**

To be completed by a government medical officer.

Pupils / Student Full name______________________________________________
Age_____________________________________________________________
Blood Count {Red and White}_____________________________________________
Stool Examination _____________________________________________________
Urinalysis _________________________________________________________
Syphilis Test _______________________________________________________
T.B. Test _________________________________________________________
Eye Test _________________________________________________________
Ears ____________________________________________________________
Chest ___________________________________________________________
Spleen __________________________________________________________
Abdomen _________________________________________________________

Additional information: e. g. Physical defects or unpairment infections, chronic or family diseases etc__________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________________
_____________________________________________________________

**<u>TO BE COMPLETED BY A GOVERNIMENT MEDICAL OFFICER:</u>**

I certify that the above - Mentioned Pupils/Student is fit to pursue his /her Secondary School Education.

**Signature.................**
**Designation..............**

**Station.....................**

**Date........................**

OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA – TAMISEMI
SHULE YA SEKONDARI JOROJIK
FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA SHULE NA MASHARTI YAKE:

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI JOROJIK,
S.L.P. 260, **KATESH – HANANG'**

**A: MWANAFUNZI**

Mimi...................................................... nimesoma kwa makini barua ya maagizo ya kujiunga na Shule yako , Pia Sheria za Shule.
Kwa heshma na unyenyekevu mkububwa ninaikubali /* Ninikataa nafasi hiyo kwa sababu
.........................................
Pia nayakubali */ Nayakataa Masharti na Sheria za Shule yako.

................................ ..............................
Tarehe Sahihi ya mwanafunzi

**B: MZAZI/ MLEZI:**

Mimi ................................................. mzazi / mlezi wa .........................................

Ambaye amechaguliwa kujiunga na Shule yako. Nime soma maagizo ya kujiunga na Sheria zake. Ninakubali */ Ninakataa nafasi hiyo, nina ahidi kumtimizia Mtotowangu mahitaji na maagizo yote ya kujiunga na Shule katika muda ulio pangwa.

Aidha naahidi kushirikiana daima na uongozi wa Shule katika kumkuza na kumlea mototo huyu kwa manufaa ya yake binafsi, wazazi na Taifa kwa ujumla.

Kama unakataa eleza sababu:-

----------------------------------------------------------------------------------------------------
----------------------------------------------------------------------------------------------------
----------------------------------------------------------------------------------------------------
----------------------------------------------------------------------------------------------------
------------------------------------------------------------------

*Ahsante.*

Jina na anuani ya mzazi/ mlezi.......................................................
.......................................................
.......................................................
.......................................................

Tarehe............................... Sahihi.......................

Futa lisilohusika.